## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI NOVEMBA, 2023 NA MWELEKEO KWA MWEZI DISEMBA, 2023.

**Dondoo za tathmini ya Novemba, 2023 na mwelekeo wa Disemba, 2023:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Novemba, 2023 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Disemba, 2023 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2023 maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka yalipata mvua za juu ya wastani ukilinganisha na wastani wa muda mrefu wa mvua za mwezi Novemba. Aidha, vipindi vya mvua kubwa zilizopelekea kutokea kwa mafuriko vilijitokeza katika baadhi ya maeneo. Kwa upande mwingine, vipindi vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka ikiashiria kuanza kwa mvua za Msimu, 2023/2024.


ii. Katika kipindi cha mwezi Disemba 2023, mvua zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi ya nchi. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI NOVEMBA, 2023.

Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2023 vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo viliripotiwa katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (ukanda wa ziwa Victoria, pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki) yalipata mvua za juu ya wastani ukilinganisha na wastani wa muda mrefu wa mvua za mwezi Novemba. Aidha, vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka ikiashiria kuanza ka mvua za Msimu 2023/2024. Vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza pia kwa baadhi ya maeneo na kusababisha athari ikiwemo mafuriko, uharibifu wa mali na miundombinu pamoja na kuathiri baadhi ya shughuli za kiuchumi. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 185.0 kilipimwa katika kituo cha hali ya hewa Lyamungu (mkoa wa Kilimanjaro) mnamo tarehe 01 Novemba, 2023, ikifuatiwa na milimita 146.1 katika kituo cha Zanzibar mnamo tarehe 5 Novemba, 2023 na Tanga (milimita 134.0) mnamo tarehe 15 Novemba, 2023. Vituo vilivyopima mvua milimita 70 au zaidi ni kama inavyoonekana katika kielelezo

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

namba 1. Kwa upande mwingine, hali ya joto la wastani hadi juu kiasi ya wastani iliendelea kujitokeza nchini katika kipindi cha mwezi Novemba, 2023.




Kielelezo 1: Vituo vilivyopima viwango vya mvua milimita 70 au zaidi katika mwezi Novemba, 2023

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI DISEMBA, 2023

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Disemba, 2023 joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki, ikiashiria kuendelea kuwepo kwa hali ya El Niño. Aidha, joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuendelea kuwa la juu ya wastani, wakati eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha uwepo wa upepo wenye unyevu unaovuma kuelekea ukanda wa pwani pamoja na mikoa ya jirani. Hali ya joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani inatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango hafifu wa kusababisha upepo wenye unyevu kutoka misitu

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

ya Congo kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa Afrika inatarajiwa kupungua nguvu kiasi na kupelekea Ukanda mvua (ITCZ) kusogea kuelekea kusini.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI DISEMBA, 2023

Katika kipindi cha mwezi Disemba 2023, mvua zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini. Kwa upande mwingine, hali ya joto kiasi inatarajiwa kuendelea hususan katika baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa, hususan katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa kati wiki ya kwanza na ya nne ya mwezi.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika maeneo mengi. Ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi ya mwezi.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa, hususan katika wiki ya kwanza ya mwezi.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo kwa vinatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa, hususan wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI JANUARI, 2024

Katika kipindi cha mwezi Januari, 2023 vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini.

## 2.4 USHAURI

Mvua zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza, hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zitakazojitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Disemba, 2023 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz